# أثر الإيمان
# في تحرير الإنسان

( باللغة السواحلية )

## تأليف

## الدكتور/ عمر سليمان الأشقر

## ترجمة

## امبوانا أحمد أوراري


Conveying Islamic Message Society
P.o.Box 834 - Alex - Egypt
E-Mail:info_en@islamic-message.net
E-Mail:cims_eg@yahoo.com
Site: www.islamic-message.net
Not for sale



شبكة الألوكة
www.alukah.net

# ATHARI YA IMANI
# KATIKA
# KUMKOMBOA MWANADAMU

Mtunzi

Dr. Omar Suleiman Al-ashqar

Mfasiri

Mbwana Ahmad Urari

شبكة الألوكة
www.alukah.net

# ATHARI YA IMANI

www.alukah.net
شبكة الألوكة

## KATIKA

# KUMKOMBOA MWANADAMU

**Mtunzi**

**Dr. Omar Suleiman Al-ashqar**

**Mfasiri**

**Mbwana Ahmad Urari**

# أثر الإيمان في تحرير الإنسان

**تاليف**

الدكتور/ عمر سليمان الأشقر

**ترجمة**

امبوانا أحمد أوراري

شبكة الألوكة - قسم الكتب

بسم الله الرحمن الرحيم

www.alukah.net
شبكة الألوكة

# UHURU NA UTUMWA

Sifa njema anazistahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, na rehema na amani zimfikie (Mtume) aliyeletwa akiwa ni rehema kwa walimwengu wote. Pia rehema na amani ziwafikie Jamaa na Swahaba wake na kila ambaye atafuata mwongozo na mwenendo wake mpaka Siku ya Malipo.

Bila shaka, neno UHURU lina utamu katika midomo na lina ladha katika masikio. Linapotamkwa neno hilo, linasisimua nafsi shupavu. Watu walio huru huona uchungu wanapokosa uhuru. Uhuru kwa wanadamu ni nyimbo ambayo, tangu zamani, hawajaacha kuiimba. Washairi wameiimba, wasuluhishi na viongozi wa mataifa mbali mbali wametoa miito ya kuufikia uhuru. Mbinu na mikakati ya kuutafuta uhuru na kujikwamua kutoka katika utumwa iliwekwa. Mataifa katika kuutafuta uhuru, yametoa mali na roho. Siku ambayo uhuru unapatikana, inafanywa sikukuu. Vyovyote

شبكة الألوكة - قسم الكتب

utakavyopekua kurasa za historia na kuyatazama maisha, hutakuta taifa linaloiona tamu ladha ya utumwa na kuuchukia uhuru.

Lakini duara la utumwa ambao watu wanaukimbia ni finyu sana. Wanadhani kuwa wakilliepuka duara hilo ndio wameepukana na utumwa, wakati ambapo sivyo mambo yalivyo. Pamoja na kuwa wanadamu wameukimbia utumwa huo wanaoudhania, utawaona bado wamo katika minyororo ya utumwa huku wakitojitambua, na wanazisherehekea sikukuu za uhuru wakati ambapo wao wenyewe wamezama katika kutekwa na utumwa!

Utumwa ambao watu wanauchukia ni ule unaomfanya mtu amilikiwe na mtu mwengine kiasi cha kumfanya awe ni bidhaa inayoweza kuuzwa na kununuliwa bila ya yeye kuwa na uwezo wowote.

Watu wanahesabu kuwa ni miongoni mwa utumwa taifa au kikundi cha watu fulani kulinyanyasa taifa au kikundi cha watu wengine. Baadhi ya jamii za binadamu katika nyakati mbali

شبكة الألوكة - قسم الكتب

mbali hazikuacha kuwafanyia dhulma baadhi nyingine. Mwenye nguvu humfanya mnyonge kuwa mtumwa, anayeshinda anamdhalilisha aliyemshinda na kumtumia katika maslahi yake; anampora matunda ya jasho lake na kheri za nchi yake. Hali ya wenye nguvu kuwanyanyasa wanyonge, wakati mwingine, hufikia kiwango cha kuwachinja wanaume na watoto."**Hakika, Firauni alijitukuza katika nchi (ya Misri) na kuwafanya watu wake makundi, akilidhoofisha kundi miongoni mwao; akiwachinja watoto wao wa kiume na kuwaacha hai watoto wao wa kike. Hakika, yeye(Firauni) alikuwa ni miongoni mwa watu waovu**". Sura Al-qasas (28), aya 4.

Ulimwengu wetu wa sasa nao haujaepukana na laana hii, japokuwa huifinika kwa jalada zuri linalovutia. Mataifa yenye nguvu katika wakati huu yanayafanya mataifa manyonge kuwa watumwa wao kwa visingizio vya maendeleo na kuyashika mkono ili eti yaendelee.

شبكة الألوكة - قسم الكتب

Na sisi Waislamu balaa hili limetukumba. Maadui zetu wametuzonga na kuuangamiza utawala wa Othman (Othman Empire), wamezigawa nchi za Kiislamu, wamepora mali zetu, wameua watu wetu, wametunyanyasa sana na bado dhulma inatuandama kila tulipo. Mateso wanayoyapata Waislamu huko Palestina, Afghanistan, India, Philippines na Ethiopia ni ushahidi wa wazi juu ya balaa hili. Aina hii ya utumwa wa binadamu kuwakalia juu binadamu wenzao, wanaipinga wale iliowapata na wanatoa juhudi katika kujinasua nayo, japokuwa wapo wenye nafsi dhaifu ambao wako radhi kudhulumiwa na kuishi maisha ya kinyama.

Pamoja na hayo, lakini kuna aina nyingine za utumwa ambazo binadamu wanazipapatikia na kutoa kila walichonacho ili kuzipata na kuzing'ang'ania sana.

Utumwa wa zamani ulikuwa ni wa kuziabudu na kuzifuata dhana na fikra zisizokuwa sahihi. Mtu ambaye hakuwa akijua hakika (fact) ya vitu vilivyokuwa katika mazingira yake, alikuwa

شبكة الألوكة - قسم الكتب

akiuogopa usiku unapoingia. Mwezi nao unapong'ara na kuangaza usiku, unakuwa kitu kikubwa sana katika nafsi yake. Jua linapochomoza na kufuta giza la usiku, mwangaza wa mwezi na nyota, inakuwa kitu kikubwa sana nafsini mwake. Anasimama kando ya milima mikubwa na mirefu na anajiona katika nafsi yake kuwa yeye ni duni. Anasimama ufukweni mwa bahari yenye kina kirefu huku mawimbi yaliyo kama milima yakifoka, na mandhari hiyo inamtisha. Woga na taadhima kwa viumbe hivi ni mambo yaliyokuwa yakimtawala binadamu wa zamani na kumfanya awe na dhana kadhaa. Ujinga wake ulimdhanishia kuwa viumbe hivyo vina haki ya kutukuzwa na kunyenyekewa na, kwa sababu hiyo, alivisujudia, aliviadhimisha na kuviomba. Lau kama atatokea mwenye akili timamu na kujaribu kumfahamisha ukweli ulivyo, ataziba masikio yake, atafumba macho yake na ataendelea kuuang'ang'ania uono wake batili. Hali hii ya kutaka kumuelimisha kama itaendelea, atachomoa panga lake na kuwa tayari kutoa nafsi na mali yake

شبكة الألوكة - قسم الكتب

akiitetea itikadi yake potofu iliyobuniwa na mawazo tasa na kusisitizwa na dhana danganyifu.

Katika kila kizazi cha wanadamu, Mwenyezi Mungu amewatuma wajumbe wake (Mitume) ili wakawaokoe wanadamu kutoka katika utumwa wa aina zote. Hii ni moja tu ya aina za utumwa uliowatawala wanadamu kwa kipindi kirefu ambapo wanadamu wameyafanya baadhi ya mandhari ya maumbile (views of nature) kuwa ni miungu wanaoabudiwa badala ya Mwenyezi Mungu. Mandhari haya katika mantiki ya Uislamu ni dalili kubwa zinazofahamisha uwezo wa Mwenyezi Mungu, na zimetenzwa nguvu, zimeumbwa, zinzmtii Mola wake na hazimuasi katika jambo lolote. Mwenyezi Mungu aliziumba mbingu na ardhi halafu akaziambia kuwa: "**....njooni mkipenda msipende. Zikasema (mbigu na ardhi): Tumekuja tukiwa watiifu**". Sura Fussilat (41), aya 11. Viumbe hivi vinamwabudu Mwenyezi Mungu, na kwa hiyo vinamtukuza na kumsujudia kwa namna tusiyoifahamu."**Na hakuna kitu chochote isipokuwa tu kinatakasa kwa kumsifu yeye (Mwenyezi**

شبكة الألوكة - قسم الكتب

**Mungu) na lakini kutakasa huko hamkufahamu**" Sura Al-israa (17), aya 44. "**Hivi huoni kuwa vinamsujudia yeye Mwenyezi Mungu vilivyomo katika mbingu na vilivyomo katika ardhi na (linamsujudia yeye) jua na mwezi na nyota na milima na miti na wanyama na watu wengi? Na (watu) wengi imawathibitikia adhabu(ya Mwenyezi Mungu). Na yeyote ambaye Mwenyezi Mungu amemfedhehesha, hakuna wa kumpa heshima. Kwa yakini, Mwenyezi Mungu hufanya atakayo**". Sura Al-hajj (22), aya 18.

Mwenyezi Mungu alimtuma Ibrahim baba wa Mitume, amani ya Mwenyezi Mungu imfikie, aende kwa watu waliokuwa wakiabudu nyota, mwezi na jua, na aliwathibitishia kuwa vitu wanavyoviabudu havina haki ya kuabudiwa, kwa sababu havikuwa na sifa yoyote ya uungu na ubwana." **Na kama hivyo tunamuonesha Ibrahim ufalme wa mbinguni na ardhini na ili awe miongoni mwa waumini. Na wakati usiku ulipomfikia (Ibrahim) aliona nyota akasema: Huyu ni Mola wangu, na wakati (nyota) ilipopotea akasema: Siwapendi miungu**

شبكة الألوكة - قسم الكتب

**wanaopotea. Na alipouona mwezi ukichomoza alisema: Huyu ni Mola wangu, na mwezi ulipozama alisema: Mola wangu asiponiongoza, nitakuwa miongoni mwa wapotevu. Na wakati alipoliona jua likichomoza alisema: Huyu ni Mola wangu. Mola huyu ni mkubwa zaidi. Jua lilipotua alisema: Enyi jamaa zangu, hakika ya mimi najitenga na hivyo mnavyovishirika (na Mwenyezi Mungu). Hakika, mimi ninauelekeza uso wangu kwa (Mwenyezi Mungu) ambaye ameumba mbingu na ardhi nikiziacha dini zote potofu, na mimi sio miongoni mwa washirikina. Na jamaa zake (Ibrahim) walijadiliana naye (wakimtahadharisha kuwa atapata madhara iwapo hatafanya kama wafanyavyo). Akasema: Hivi mnajadiliana na mimi juu ya Mwenyezi Mungu na ilhali yeye ameniongoza? Na siviogopi mnavyovishirikisha naye (kuwa eti vitanidhuru kama sitaviabudu) isipokuwa tu (namuogopa) Mola wangu (ambaye) akitaka jambo (liwe, ndilo linalokuwa). Mola wangu anakijua vyema kila kitu. Hivi hamzinduki?**". Sura Al-an'aam (6), aya 75-80.

شبكة الألوكة - قسم الكتب

Wanadamu walitumbukia pia katika shimo jingine katika uwanja wa dhana potofu pale walipoabudu masanamu viziwi, bubu, yasiyokuwa na uhai, na pale walipowaabudu watu waliokufa na ambao hawana uwezo wa kudhuru wala kunufaisha na wasiomiliki uhai, mauti na kufufua. Watu walikuwa wakiyatengeneza masanamu kwa mikono yao halafu wanayaomba na kuyanyenyekea. Wanamfukia maiti katika mchanga kwa mikono yao halafu wanamuomba msaada na kuzielekeza kwa maiti huyo nia na ibada zao. Mwenyezi Mungu aliwatuma wajumbe wake ili wawakomboe wanadamu kutoa katika uchafu huu ambao uliwafanya wawe watumwa wa miti, mawe na maiti. Mitume, katika harakati zao za kuwaelimisha wanadamu, walitoa juhudi kubwa. Walijadiliana nao, waliwapigia mifano na waliyavumilia maudhi yao. " **Alisema (Ibrahim kuwaambia watu wake waliokuwa wakiabudu masanamu kuwa): Hivi (masanamu haya) yanakusikieni wakati mnapoyaomba? Au yanakunufaisheni(mnapoyaabudu)? Au**

شبكة الألوكة - قسم الكتب

**yanakudhuruni (msipoyaabudu? Wakasema: (masanamu haya hayatunufaishi wala hayatudhuru) Bali tumewakuta wazee wetu wanafanya hivy (ndio na sisi tukafuata**". Sura Ash-shuaraa (26), aya 72-74. "**Enyi watu, unapigwa mfano, usikilizeni. Hakika, wale mnaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu hawawezi kuumba (hata) nzi, japo wangejumuika kwa ajili ya hilo. Na kama nzi atawapora kitu, basi hawawezi kukikomboa. Amekuwa dhaifu aliyenyang'anya (nzi) na anayenyang'anywa (masanamu)**". Sura Al-hajj (22), aya 73.

Pamoja na jitihada za Mitume za kutaka kuwaelimisha wanadamu, bado wengi waliendelea kuing'angania batili hii na kuamua kubaki kuwa watumwa wa masanamu, maiti na kuahidi kwamba wataendelea kuwa wavumilivu juu ya itikadi zao batili. "**Na walisema (viongozi wa watu wa Nabii Nuuh kuwaambia wafuasi wao kuwa): Msiiache miungu yenu; na msiache Wadd wala Suwaa na Yaghuuth na Yauuq na Nasr**". Sura Nuuh (71), aya 23. "**Na liliondoka kundi katika wao (waliokuwa**

شبكة الألوكة - قسم الكتب

**wakisikiliza mafunzo ya Mtume na kuwaambia wenzao kuwa): Ondokeni (msimsikilize Mtume), na endeleeni kuabudu miubgu yenu. Hakika, hili (la kukatazwa kuabudu miungu yenu) ni jambo lililokusudiwa (kuivunja dini yenu**". Sura Saad (38), aya 6. Watu waliziba masikio yao ili sauti ya haki isifike kwenye nyoyo zao. "**Na (alisema Nabii Nuhu): Hakika, mimi kila nilipokuwa nikiwalingania ili upate kuwasamehe, waliweka vidole vyao katika masikio yao, na walijifinika nguo zao na waling'ang'ania (ibada zao) na walifanya kiburi kikubwa**". Sura Nuuh (71), aya 7.

Wanadamu waliwafanya wanadamu wenzao kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu. Waliwapachika baadhi ya watu sifa za uzushi na hivyo kuwafanya watu hao kuwa wanatokana na kizazi cha miungu. Walidai kuwa watu hao wana maumbile tofauti na maumbile ya watu wengine, na kwamba katika mishipa yao ya damu inatembea damu ya rangi ya bluu. Baadhi ya watu hao walioabudiwa walikuwa ni:

شبكة الألوكة - قسم الكتب

1. Wafalme waliotaka kuwafanya watu wawe wanyenyekevu na watiifu wa matakwa yao.
2. Watu wema waliotukuzwa na watu bila ya wao wenyewe kutaka kutukuzwa namna hiyo.

Miongoni mwa mfano wa kundi la kwanza ni Firauni ambaye alidai uungu pale alipowakusanya watu wake na kuwatangazia kuwa: "**Mimi ndiye Mola wenu mkubwa zaidi**". Sura An-naaziaat (79), aya 24. "**Sijui kuwa mnaye Mungu (mwengine) asiyekuwa mimi**". Sura Al-qasas (28), aya 38.

Miongoni mwa mfano wa kundi la pili ni wale watu waliopituka mipaka katika kumtukuza Mtume Issa na hivyo kudai kuwa Mungu au Mwana wa Mungu au Wa Tatu kati ya Miungu Watatu. Ametakasika Mwenyezi Mungu na hayo wanayoyasema kutakasika kukubwa.

Mwenyezi Mungu aliwatuma Manabii wake ili wawakomboe wanadamu kutoka katika utumwa wa kuwaabudu wanadamu wenzao. Mwenyezi Mungu alimtuma Mtume Mussa na ndugu yake Haarun waende kwa Firauni na watu wake na kuwaambia: "**Nendeni kwa Firauni, kwani amepituka mipaka.**

شبكة الألوكة - قسم الكتب

**Mwambieni maneno mazuri huenda akaonyeka au akaogopa**". Sura Taahaa (20), aya 43-44. Walimtaka awaachie huru Wana Wa Israili. "**Mwendeeni (Firauni) na mwambieni: Sisi ni Wajumbe wa Mola wako, hivyo, waache wawe nasi Wana Wa Israili na usiwatese**". Sura Taahaa (20), aya 47. Mwenyezi Mungu alimtaka Firauni aache kiburi chake, awe mnyenyekevu kwa Mola wa walimwengu, awaache huru Wana Wa Israili watoke katika madhila ya utumwa na awaruhusu waondoke nchini mwake.

Qur'an yetu imetuhadithia habari za Mtume Issa. Aliyakanusha waliyoyadai waliodai kuhusu suala lake. Alithibitisha kuwa yeye ni Mja wa Mwenyezi Mungu, ni Mjumbe wake, ni Neno lake alilolifunua kwa (mama yake) Maryam na ni Roho kutoka kwake. Mfano wake katika hilo ni kama mfano wa Adamu aliyeumbwa kutokana na mchanga halafu akauambia: Kuwa (mwanadamu), naye akawa (mwanadamu) kama Mwenyezi Mungu alivyotaka awe.

شبكة الألوكة - قسم الكتب

Wanadamu walitumbukia katika utumwa wa aina nyingine. Aina hii ni utumwa wa kuabudu mifumo na fikra. Akili za watu wenye vipaji na wanafalsafa katika kila zama huwa zinavumbua nadharia, mifumo, kanuni na misingi wanayoifanya kuwa sheria kwa wanadamu wenzao. Mifumo na kanuni hizo huwa zinapingana na sheria za Mwenyezi Mungu wakati Mwenyezi Mungu anataka sheria zinazowahukumu watu ziwe mikononi mwake na si kwa mwengine. "**Haikuwa hukumu ila ni ya Mwenyezi Mungu tu. Ameamrisha kuto(mw)abudu yeyote ila yeye tu**". Sura Yusuf (12), aya 40. Mwenyezi Mungu wa haki hayuko radhi kuona yeyote akifanywa mshirika pamoja naye katika sheria zake "**Na hamshirikishi yeyote katika sheria zake**". Sura Al-kahf (18), aya 26.

Mwenyezi Mungu amewashutumu Wayahudi na Wakristo ambao waliwatii wanachuoni na watawa wao pale walipozipinga sheria walizokuwa nazo, hivyo wakahalalisha na kuharamisha kwa maoni yao. Amewaelezea kuwa: "**Waliwafanya wanazuoni wao na watawa wao kuwa ni miungu**

شبكة الألوكة - قسم الكتب

**badala ya Mwenyezi Mungu na Masiah Mwana wa Maryam (pia wamemfanya kuwa ni Mungu)**". Sura At-tawba (9), aya 31.

Lakini jambo la ajabu ni kwamba watu wengi sana wanakataa mfumo na sheria za Mwenyezi Mungu na kuziridhia kanuni na sheria za wanadamu ambazo zinawafanya wawe watumwa wa wanadamu wenzao. Misingi na kanuni za wanadamu zinatofautiana na zinapingana. Kila kundi linadai kuwa liko katika haki na kwamba mfumo wake ndio unaomkomboa mwanadamu na kumletea kheri na raha. Hutokea mpambano kati ya wafuasi wa mifumo, na aghlabu huishia kwenye vita vinavyoangamiza kila kitu. "**Na Wayahudi walisema (kuwa): Wakristo hawana lolote. Na Wakristo (nao) walisema (kuwa): Wayahudi hawana lolote, na ilhali wao (wote) wanasoma vitabu. Kama hivyo walisema wale ambao hawajui (kitu) mfano wa maneno yao. Mwenyezi Mungu atahukumu kati yao**". Sura Al-baqara (2), aya 113.

شبكة الألوكة - قسم الكتب

Mwenyezi Mungu katika kila zama ameteremsha vitabu ili vihukumu baina ya watu katika yale wanayotofautiana, na hivyo kuweka haki na kubatilisha batili. "**Watu walikuwa ni umma mmoja. Mwenyezi Mungu akatuma Mitume wanaotoa habari njema na wanaotoa habari za maonyo, na pamoja nao akateremsha vitabu kwa haki ili vihukumu baina ya watu katika yale waliyotofautiana. Na hawakutofautiana katika hayo isipokuwa tu wale waliopewa vitabu hivyo baada ya kuwafikia hoja zilizo wazi, kwa sababu ya husda kati yao. Mwenyezi Mungu akawaongoza walioamini kwenye kuifuata haki katika yale waliyotofautiana, kwa idhini yake. Na Mwenyezi Mungu anamuongoza amtakaye kwenye njia iliyo nyooka**". Sura Al-baqarah (2), aya 213.

Qur'an imewaita watu waliopewa vitabu (Wayahudi na Wakristo) kwenye kumwabudu Mungu mmoja, wa pekee na kuwaacha washirika wanaowaabudu. Kwa kufanya hivyo, watu watakuwa wamejumuika katika tamko moja lililo sahihi. "**Sema: Enyi mliopewa vitabu, njooni**

شبكة الألوكة - قسم الكتب

**kwenye tamko lililo sawa baina yetu na baina yenu kwamba tusi(mw)abudu (yeyote) ila Mwenyezi Mungu tu, na tusikishirikishe naye kitu chochote, na baadhi yetu wasiwafanye baadhi nyingine kuwa miungu badala ya Mwenyezi Mungu. Iwapo watakataa, semeni (muwaambie kuwa): Shuhudieni kuwa sisi ni Waislamu (watiifu)**". Sura Aal-imraan (3), aya 64.

Uislamu umekuja ili uwakomboe wanadamu watokane na utumwa wa kuwaabudu wanadamu wenzao, wawe wakimwabudu Mwenyezi Mungu pekee. Walinganiaji wa mwanzo waliutangaza ukweli huu walipokuwa wakienda kukutana na viongozi wa Kirumi na wa Kiajemi. Viongozi hao walikuwa wakiwauliza walinganiaji kuhusu lengo lililowatoa katika nchi zao, na wahubiri walijibu kuwa: "**Mwenyezi Mungu ametutuma ili tuwatoe watu katika kuwaabudu wanadamu (wenzao) wawe wakimwabudu Mwenyezi Mungu, na tuwatoe katika udhalimu wa dini (potofu) waingie katika uadilifu wa Uislamu, na tuwatoe katika dunia finyu waelekee kwenye akhera pana**".*

شبكة الألوكة - قسم الكتب

Jambo muhimu sana ambalo Uislamu unalihangaikia ni kuukomboa moyo wa mwanadamu uondokane na utumwa huo (wa mwanadamu kumwabudu mwanadamu mwenzie). Moyo ndio nguzo ya msingi inayouongoza mwili wote, kuuendesha na kuuelekeza. Kwa kuwa mwema moyo, ndio mwanadamu anakuwa mwema. Kuhusu hilo, anasema Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kuwa: "**Ee, katika mwili kuna kipande cha nyama. Kinapokuwa chema, mwili wote unakuwa mwema. Na kinapokuwa kiovu, mwili wote unakuwa muovu. Ee, kipande hicho cha nyama ni moyo**".

Moyo ndio mahali pa itikadi, hima, utashi na nia. Kwa kuwa njema itikadi na utashi, ndio moyo unakuwa mwema na kwa kuwa mwema moyo ndio mwanadamu anakuwa mwema.

Itikadi inakuwa njema kwa kumtambulisha mja Mola wake na siafa zake, majina yake, vitendo vyake, malaika wake, Siku ya Mwisho na mambo

شبكة الألوكة - قسم الكتب

aliyoyaandaa Mwenyezi Mungu katika siku hiyo kwa mwenye kumtii na mweye kumuasi.

Nia inakuwa njema kwa mtu kumkusudia Muumba wake katika matendo yake yote. Asimkusudie kwa matendo yake malaika, mfalme, mti, jiwe wala mwanadamu. Huu ndio utakaso (ikhlaas) katika kuabudu, utakaso ambao

---

* Maneno hayo yalisemwa na Rib-iy bin Aamir kumwambia Rostom kiongozi wa Waajemi. Angalia kitabu Al-bidaaya Wan-nihaaya cha Ibn-kathiir, Yaliyotokea mwaka wa 14, Vita vya Qaadisiyya.

Mwenyezi Mungu haikubali dini ya mtu yeyote isiyokuwa na utakaso huo. "**Basi mwabudu Mwenyezi Mungu ukimtakasia yeye tu dini**". Sura Az-zumar (39), aya 2. "**Basi muombeni yeye mkimtakasia yeye tu dini**" Sura Ghaafir(Al-muumin 40), aya 65. "**Ee, ni ya Mwenyezi Mungu tu dini takasifu**". Sura Az-zumar (39), aya 3. Utakaso ndio

شبكة الألوكة - قسم الكتب

maana ya Laa ilaaha il-lallaah (Hakuna mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu tu). Kwa kufanikisha utakaso, ndio mja anakuwa ameufanikisha umja wake kwa Mola wake.

Uislamu unakusudia pia kuukomboa moyo wa mwanadamu uondokane na kuiogopa miungu bandia, mashetani na madhalimu. Hofu inalemaza harakati, fikra na utashi wa mwanadamu na kumfanya awe sio mja(mtumishi) wa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu anasema: Mimi ndiye mtukufu, mkubwa, mwenye ufalme, mwenye nguvu kubwa, mbabe, nina jeshi la mbinguni na ardhini, hivyo, msimwogope yeyote asiyekuw mimi, na mashetani na madhalimu nao katika kila zama wanajaribu kuotesha woga katika nyoyo za waja wawaogope washirika na wafuasi wao. Huyu hapa Mtume Ibrahim wanahojiana naye watu wake na kumtisha kuwa miungu yao itamdhuru, naye anajikinga kwa Mwenyezi Mungu Mola wake. "**Na wakahojiana naye watu wake. Akasema: Hivi mnahojiana nami kuhusu Mwenyezi Mungu na ilhali yeye (ndiye) ameniongoza? Na siviogopi**

شبكة الألوكة - قسم الكتب

**mnavyovishirikisha naye (kuwa vitanidhuru) isipokuwa tu Mola wangu akitaka jambo (liwe ndilo linalokuwa). Mola wangu analijua vyema kila jambo. Je, hamuonyeki? Na vipi niviogope mnavyovishirikisha (na Mwenyezi Mungu) na ilhali nyinyi hamuogopi kuwa mnavishirikisha na Mwenyezi Mungu vitu ambavyo (yeye) hakuvishushia ushahidi (wowote) kwenu? Basi ni kundi lipi kati ya mawili (la kwangu na la kwenu) lina haki zaidi ya kuwa na amani ikiwa nyinyi mnajua? Wale ambao wameamini na wasiichanganye imani yao na ushirikina, basi wao ndio wenye amani na wao ndio wenye kuongoka. Na hizo ni hoja zetu tumempa Ibrahim ahojiane na watu wake. Tunamnyanyua daraja za juu tunayemtaka. Bila shaka, Mola wako ni mwenye hekima, mjuzi**". Sura Al-an'aam (6), aya 80-83.

Wakati Mtume Hud, Mwenyezi Mungu amfikishie amani, alipokuwa mkali katika kukabiliana na watu wake, walimwambia kuwa: "**Hatusemi isipokuwa tu baadhi ya miungu wetu wamekushushia balaa. Alisema: Mimi**

شبكة الألوكة - قسم الكتب

**ninamshuhudisha Mwenyezi Mungu na (nyinyi pia) shuhudieni kuwa mimi nimejitenga na mnavyovishirisha (na Mwenyezi Mungu) badala yake. Basi nifanyieni vitimbi (vya kunidhuru kama mnaweza nyinyi) nyote na msinicheleweshe. Mimi nimemtegemea Mwenyezi Mungu Mola wangu na Mola wenu. Hakuna kiumbe chochote isipokuwa yeye (Mwenyezi Mungu) tu ndiye mwenye kukidhibiti. Bila shaka, Mola wangu yuko katika njia iliyonyooka**". Sura Hud (11), aya 54-56.

Vipi angeweza kukabiliana na watu wake kama angeuamini uzushi walioudai kwamba miungu yao inadhuru, inanufaisha na kuwapa maadui wao matatizo na madhara? Moyo wake, Mwenyezi Mungu ampe amani, umeepukana na utumwa wa kuiabudu miungu hii batili. Kwa sababu hiyo, aliweza kuwakabili watu wake kwa aina hii kali ambayo aliwapa changamoto akimtegemea Mwenyezi Mungu Mola wake, mpenzi wake, mjuzi wa kila jambo na mwenye kuwadhibiti waja.

شبكة الألوكة - قسم الكتب

Katika kukabiliana na wababe, Mola wa waja anawaelekeza waja wake wamtegemee yeye. Mtume Mussa na Harun, Mwenyezi Mungu awafikishie amani, walimwambia Mola wao alipowaamrisha kwenda kwa Firauni kuwa: "**Hakika, sisi tunaogopa asije akapituka mipaka juu yetu au akafanya kiburi**". Sura Taahaa (20), aya 45. Mwenyezi Mungu akawaambia**: "Msiogope. Mimi niko pamoja nanyi, ninasikia na ninaona**". Sura Taahaa (20), aya 46.

Shetani huwatia hofu waja wa Mwenyezi Mungu wenye utakasifu (ikhlaas) wawaogope wafuasi wake wapotevu. Mwenyezi Mungu wa haki ametuelekeza tusiwaogope wafuasi hao wa shetani na badala yake tumwogope yeye tu. "**Hakika, hakuna vingine isipokuwa kwamba huyo ni shetani tu anakutieni hofu muwaogope marafiki (wafuasi) wake. Msiwaogope, na niogopeni mimi ikiwa nyinyi ni waumini**". Sura Aal-imraan (3), aya 175.

Moyo kufungamana na Mola wa waja pamoja na kumtegemea ni nguzo madhubuti ambayo waja

شبكة الألوكة - قسم الكتب

wema walikuwa wakiitegemea, na wanaendelea kuitegemea, katika kupambana na ufisadi, ubabe na matatizo ya maisha. Mtume Ibrahim anatumbukizwa katika moto naye anasema: "**Tosha yetu ni Mwenyezi Mungu naye ndiye msaidizi bora zaidi**". Sahih Bukhariy, Kitabu cha Tafsiri ya Qur'an, Hadithi namba 4197, 4198.

Naye Mtume Yunus anatumbukizwa baharini na kumezwa na samaki na anaita: "**Hakuna mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa wewe (Mwenyezi Mungu) tu uliyetakasika. Hakika, mimi nilikuwa miongoni mwa wenye kudhulumu (nafsi zao). Tukamjibu maombi yake na tukamuokoa kutoka katika huzuni. Na kama hivyo, tunawaokoa waumini**". Sura Al-anbiyaa (21), aya 87-88.

Mtume Nuh naye anazidiwa na maudhi ya watu wake huku akiwa amekaa nao muda mrefu na anamuomba Mwenyezi Mungu wa haki naye anamwitikia. "**Na (mkumbuke Mtume) Nuh wakati alipodangana (alipotoa sauti ya kuomba msaada) huko nyuma, tukamwitikia maombi yake, hivyo**

شبكة الألوكة - قسم الكتب

**tukamuokoa (yeye) na watu wake kutoka katika tatizi kubwa. Na tukamnusuru kutoka kwa watu ambao walizikanusha aya zetu. Hakika, wao walikuwa ni watu waovu, hivyo, tukawagharikisha (tukawaangamiza baharini) wote** ". Sura Al-anbiyaa (21), aya 76-77.

Kikundi cha waumini wachache kinalitazama jeshi kubwa likiwa limesimama pamoja na Jaluti, na kikundi hicho kinajihami kwa Mwenyezi Mungu mwenye kutoa msaada na ushindi, naye anakisaidia na kukinusuru. "**Wakati (Taluti) alipouvuka (mto) yeye na wale ambao wameamini pamoja naye, walisema: Leo hatuna uwezo wa kumkabili Jaluti na jeshi lake. Walisema wale ambao wana dhana ya yakini ya kukutana na Mwenyezi Mungu: Ni makundi mangapi machache yameweza kuyashinda makundi mengi kwa idhini ya Mwenyezi Mungu? Na Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wenye subira. Na wakati walipotoka kwa kupambana na Jaluti na jeshi lake walisema: Ewe Mola wetu, tumiminie subira na iimarishe miguu yetu na tupe ushindi juu ya watu makafiri.**

شبكة الألوكة - قسم الكتب

**Wakawashinda kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, na Daudi alimuua Jaluti, na Mwenyezi Mungu alimpa Daudi ufalme na hekima na akamfundisha aliyotaka (kumfundisha)**". Sura Al-baqara (2), aya 249 – 251.

Kundi la waumini lilisimama imara pamoja na Mtume (Muhammad), Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, katika kupambana na makafiri huko Badri, na ilhali walitoka kwa ajili ya kukabiliana na msafara wa biashara na hawakudhani kuwa watakutana na vita, na hawakujiandaa kwa ajili ya vita. Walishtukizwa na jeshi ambalo idadi yake ni mara tatu ya idadi yao. Walijiegemeza kwa Mola wao na mpenzi wao wakimuomba ushindi na msaada, naye akawapa ushindi na msaada na kushusha malaika wakipigana pamoja nao. "**(Kumbukeni) Wakati mlipomuomba Mola wenu naye akakujibuni kuwa: Hakika, mimi nitakusaidieni kwa (kukuleteeni) malaika elfu moja watakaofuatana. Na (Mwenyezi Mungu) hakulifanya hilo isipokuwa tu ni habari njema na ili nyoyo zenu ziwe tulivu kwalo. Na ushindi hautoki**

شبكة الألوكة - قسم الكتب

**ila kwa Mwenyezi Mungu tu. Hakika, Mwenyezi Mungu ni mwenye nguvu, mwenye hekima. (Kumbukeni) Wakati alipokuleteeni usingizi ukiwa ni amani kutoka kwake na kukushushieni kutoka mawinguni maji(mvua) ili akutoharisheni kwayo na kukuondosheeni uchafu wa shetani na kuzipa nguvu nyoyo zenu na kuiimarisha kwayo miguu (yenu). (Kumbukeni) Wakati Mola wako alipowafunulia malaika kwamba: Mimi niko pamoja nanyi hivyo, waimarisheni wale ambao wameamini. Nitatia hofu katika nyoyo za wale ambao wamekufuru. Hivyo, pigeni juu ya shingo na pigeni kwao kila ncha ya kidole. Hayo ni kwa sababu wao walimpinga Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na yeyote anayempinga Mwenyezi Mungu na Mtume wake basi Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu**". Sura Al-anfaal (8),aya 9-13.

Baada ya Kuwapata Waislamu yaliyowapata katika vita vya Uhud, Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, aliwaamrisha Swahaba wake wapiganaji, pamoja na majeraha waliyokuwa

شبكة الألوكة - قسم الكتب

nayo, wawafuatilie makafiri, nao walitii. Uliwapitia msafara ambao nao uliwapitia Waquraish na ilhali wakijadiliana juu ya kuwarudia Waislamu ili kuwamaliza. Msafara huo ulipowapa habari Waislamu, halikuwavunja moyo jambo hilo na walitamka maneno yaliyotamkwa na waja wema kuwa: Tosha yetu ni Mwenyezi Mungu tu, naye ni msaidizi bora zaidi. "**Wale ambao wamemuitikia (wamemkubalia) Mwenyezi Mungu na Mtume baada ya kuwa wamepata majeraha. Wale waliofanya yaliyo mazuri katika wao na kumcha Mwenyezi Mungu, watapata malipo makubwa. Ambao watu (msafara wa kibiashara) waliwaambia kuwa: Kwa yakini, watu (Waquraish) wamekukusanyieni (kila aina ya silaha ili kukumalizeni) hivyo waogopeni. (Lakini) Hilo liliwazidishia imani na kusema: Tosha yetu ni Mwenyezi Mungu tu, naye ni msaidizi bora zaidi. Wakarudi (vitani) na neema na fadhila za Mwenyezi Mungu. Hawakuguswa na ubaya wowote, na walizifuata radhi za Mwenyezi Mungu,**

شبكة الألوكة - قسم الكتب

**na Mwenyezi Mungu ni mwenye fadhila kubwa**". Sura Aal-imraan (3), aya 172-174.

Makafiri katika vita vya Khandaq waliuzingira mji wa Madina. Wayahudi walivunja mikataba yao na Waislamu. Wanafiki walitangaza uvumi wa kuvunja moyo. Waislamu walipata mshtuko mkubwa, lakini moyo wa Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, na mioyo ya wale waliokuwa wakimfuata vizuri Mtume iliendelea kuwa na uhusiano na Mwenyezi Mungu. Mtume alikuwa akiuona ushindi ndani ya makundi ya makafiri si katika vita hivyo tu bali ushindi kwa mataifa makubwa; Warumi na Wapeshia. "**Enyi ambao mmeamini, ikumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu juu yenu wakati yalipokujieni majeshi tukyapelekea upepo na majeshi (ambayo) hamkuyaona. Na Mwenyezi Mungu amekuwa ni mwenye kuyaona mnayoyatenda. Wakati (majeshi hayo) yalipokujieni juu yenu na chini yenu na wakati macho yalipokodoka na mioyo ikafika kooni na mkamdhania Mwenyezi Mungu dhana mbali mbali. Hapo, Waislamu walipata mtihani na**

شبكة الألوكة - قسم الكتب

**kutingishwa mtingisho mkubwa. Na (kumbuka) wakati wanafiki na wale ambao katika mioyo yao kuna ugonjwa waliposema kuwa: Mwenyezi Mungu na Mtume wake hawakutuahidi isipokuwa hadaa tu. Na (kumbuka) wakati kundi katika wao liliposema kuwa: Enyi watu wa Yathrib (Madina) Hamna pa kukaa hivyo, rudini. Na (kumbuka wakati) kundi (jingine) katika wao likimuomba ruhusa Mtume (ya kurudi na kutoingia vitani) na kusema: Kwa yakini, nyumba zetu ziko tupu (hakuna wa kuzilinda), na hazikuwa tupu. Hawakutaka isipokuwa kukinmbia (vita) tu**". Sura Al-ahzaab (33), aya 9-13.

Katika hali hii ngumu, Mtume na Swahaba wake watukufu walisimama imara kwa sababu waliamini ushindi wa Mwenyezi Mungu na ahadi yake. "**Kwa yakini, mmekuwa na kiigizo chema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anayemtaraji Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na kumkumbuka sana Mwenyezi Mungu. Na wakati waumini walipoyaona makundi (ya maadui) walisema: Haya ndio yale aliyotuahidi Mwenyezi**

شبكة الألوكة - قسم الكتب

**Mungu na Mtume wake, na amesema kweli Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na hilo halikuwazidishia isipokuwa tu imani na utii**". Sura Al-ahzaab (33), aya 21-22.

Mwenyezi Mungu wa kweli amewasifu watu hawa wema kwa kusema: "**Katika waumini kuna watu walioyasadikisha yale waliyomuahidi Mwenyezi Mungu. Katika wao kuna waliokufa, na katika wao kuna wanaongojea na hawakubailisha kabisa (ahadi yao)**". Sura Al-ahzaab (33), aya 23.

Waumini waliouamini msaada wa Mwenyezi Mungu walirudi vitani wakiwa na malipo makubwa, na wanafiki walirudi wakiwa na fedheha na nyuso nyeusi wakati makafiri walikimbia huku nyoyo zao zikiwa na hasira na machungu. "**Ili Mwenyezi Mungu awalipe wakweli kwa ukweli wao na awaadhibu wanafiki akitaka au awasamehe. Kwa yakini, Mwenyezi Mungu amekuwa ni msamehevu sana, mwenye rehema sana. Na Mwenyezi Mungu akawarudisha wale ambao wamekufuru wakiwa na hasira zao hawakupata kheri yoyote. Na**

شبكة الألوكة - قسم الكتب

**Mwenyezi Mungu akawatoshea waumini vita, na Mwenyezi Mungu amekuwa mwenye nguvu, mwenye nguvu kubwa**". Sura Al-ahzaab (33), aya 24-25.

Ama wale Wayahudi ambao waliwasaidia makafiri, Mwenyezi Mungu aliwamilikisha Waislamu ardhi zao, nyumba zao, mali zao na kuwafukuza vibaya sana. "**Na (Mwenyezi Mungu) akawateremsha kutoka katika ngome zao wale waliopewa kitabu (Wayahudi) waliowasaidia maadui, na akatia hofu katika nyoyo zao. Makundi mkayaua na makundi mengine mkayateka. Na akakurithisheni ardhi yao na mali zao na ardhi ambayo hamjaikanyaga. Na Mwenyezi Mungu amekuwa ni muweza wa kila jambo**". Sura Al-ahzaab (33), aya 26-27.

Waislamu, kupitia historia yao baada ya Mtume, waliyazingatia vyema masomo haya. Watawala wema na viongozi wa kijeshi wa Kiislamu, wamekuwa wakishughulika kuwalea wanajeshi juu ya maadili ya kweli ya Kiislam na kuupa nguvu

شبكة الألوكة - قسم الكتب

uhusiano wao na Mwenyezi Mungu ili hofu yao iwe ni ya kumuogopa Mwenyezi Mungu na mapenzi yao yawe ni ya kumpenda Mwenyezi Mungu. Kwa kufanya hivyo, wanapata sababu za kupata ushindi. "**Kwa yakini, sisi tunawanusuru (tunawapa ushindi) Mitume wetu na wale ambao wameamini katika maisha ya duniani na siku watakaposimama mashahidi**". Sura Ghaafir (Al-muumin 40), aya 51.

Salaahud-din Al-ayyubi katika vita vingi alikuwa akimuulizia mtu mwema Kadhi Fadhil kama yupo. Mara nyingi moyo wake ulikuwa tulivu na hofu kuondoka pale amuonapo mtu huyo mwema akiwa amesimama kando kando ya majeshi akimuomba Mwenyezi Mungu nusra na ushindi.

Wakati alipopiga ukelele mmoja kati ya wanajeshi wa Kiislamu muda mchache kabla ya vita vya Yarmuk kuwa: " **Wingi ulioje wa Warumi, na uchache ulioje wa Waislamu?",** Khalid bin Waliid alimfokea na kumwambia "**Sema: Ni uchache ulioje wa Warumi, na wingi ulioje wa Waislamu**", na alimkumbusha kauli ya Mwenyezi Mungu wa kweli

شبكة الألوكة - قسم الكتب

isemayo kuwa "**Ni vikundi vingapi vichache vimevishinda vikundi vingi kwa idhini ya Mwenyezi Mungu**". Sura Al-baqara (2), aya 249.

Wakati kamanda wa Kiajemi alipomtisha kamanda wa jeshi la Kiislamu kwa wingi wa idadi ya jeshi la Kiajemi, kamanda wa jeshi la Kiislamu alimwambia: "**Tumekujieni na watu (wapiganaji) wanaopenda kufa kama nyinyi mnavyopenda kuishi**".

Uhusiano wa Waislamu na Mwenyezi Mungu ulipokuwa dhaifu na mawasiliano yao na Mwenyezi Mungu yakakatika na nyuso zao wakazielekeza kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu katika wakati wetu wa sasa ; mara wanaelekea Urusi, mara Amerika, mara Umoja wa Mataifa, mara Baraza la Usalama na mara Jumuiya ya Ulaya,(walipofanya hivyo) vipigo vimewaandama, maadui wao wametimiza malengo yao na wamewashinda na kuwadhalilisha. Misiba hii si lolote isipokuwa tu ni ushahidi wa kuwepo magonjwa hatari yalioupata umma wa Kiislamu. Mfano wake ni kama magonjwa mengine ambayo

شبكة الألوكة - قسم الكتب

yanaipata miili dhaifu, na mfano wake pia ni kama nyumba mbovu ambazo hazihimili pepo kali zinazovuma.

Mwenyezi Mungu wa haki ametufahamisha kuwa huwa anawaadhibu waja wake wenye kuupuuza mwongozo wake na wenye kuukimbia wahyi wake kwa kuwapa misiba na maafa ili warejee kwa Mola wao. "**Na kwa yakini kabisa, tulipeleka (Mitume) kwa mataifa yaliyokuwa kabla yako (wakakufuru) hivyo, tukawaadhibu kwa dhiki na mashaka ili wapate kunyenyekea (na kurejea kwa Mola wao)**". Sura Al-an'aam (6), aya 42.

Miongoni mwa balaa ambalo Mwenyezi Mungu huuadhibu kwalo umma ambao ameupa dhamana ya dini na wahyi wake, ikiwa umma huo utapuuza, ni panga za maadui wake waovu. Mwenyezi Mungu huwaadhibu Waislamu ambao wamepotea na halafu huwaadhibu maadui wake makafiri.. Chukua zingatio katika haya kwa kuangalia iliyoyapata umma wa Wayahudi pale Mwenyezi Mungu alipowapelekea maadui zao kwa

شبكة الألوكة - قسم الكتب

sababu ya dhuluma zao na ilhali katika Wayahudi hao kuna Mitume na watu wema. "**Hivi hukuliona kundi katika Wana wa Israili baada ya (Mtume) Musa wakati walipomwambia Mtume wao kuwa: Tuletee mfalme ili tupigane katika njia ya Mwenyezi Mungu? Akasema: Haielekei kuwa mkianadikiwa kupigana hamtapigana? Wakasema: Vipi tusipigane katika njia ya Mwenyezi Mungu na ilhali tumetolewa katika majumba yetu na watoto wetu?** ". Sura Al-baqara (2), aya 246.

Majusi (wanaoabudu moto) chini ya uongozi wa Nabukhadhnasr waliwavamia Wayahudi na kuzikalia nchi zao, kuchoma nyumba zao, kuua waliowaua na kuwateka waliowateka. Wayahudi walikaa mateka miaka sabini.

Waislamu watakaporudi kwenye kumnyenyekea Mwenyezi Mungu, kumpenda, kumuogopa, kumkusudia yeye pekee, kumtegemea na kumuomba msaada atawashushia msaada na radhi zake, na kuwaondolea hasira zake.  Katika hili, chukueni mazingatio kwa yale yanayotokea katika

شبكة الألوكة - قسم الكتب

nchi ya Afghanistan ambapo Waislamu wamesimama imara dhidi ya ukafiri na udhalimu. Wanapigana na makafiri ambao wanataka kuufuta Uislamu. Wamepigana na ilhali hawana isipokuwa mali na silaha kidogo sana. Wamepambana na taifa kubwa la kikafiri la Urusi na Mwenyezi Mungu akawapa nguvu na kuwasaidia. Walipambana na maadui wao miaka mnne na vita vingali vikiendelea. Walipata silaha zao kutoka mikononi mwa maadui wao, wamejiunga nao makamanda na wanajeshi waliopata mafunzo na ambao ni wananchi wenzao, wamedondosha mamia ya ndege, wameharibu maelfu ya vifaru na kuua maelfu ya maadui wa Mwenyezi Mungu. Wapiganaji (Mujahidin) waaminifu wamesimulia huko miujiza mikubwa ambayo kwayo Mwenyezi Mungu amelipa nguvu jeshi lake na kuwadhalilisha makafiri. Idadi chache ya Mujahidin imeyashinda majeshi makubwa. Silaha hafifu zimeangamiza silaha za kisasa. Hayo hayakupatikana isipokuwa tu ni kutokana na msaada wa Mwenyezi Mungu ambao kwao amelisaidia jeshi la Kiislamu.

شبكة الألوكة - قسم الكتب

Vita vya Jihadi vya Afghanistan ni mawaidha kwa Waislamu wazembe katika wakati wetu wa sasa. Tunawaambia kuwa: Kwa yakini, kuna nguvu nyingine isiyokuwa ya mataifa makubwa inayoweza kubadilisha mwelekeo wa vita, lakini tu inahitaji waumini ambao watajitoa muhanga katika kutetea na kuiendeleza dini ya Mwenyezi Mungu na kumfanya Mwenyezi Mungu kuwa mtetezi wao. Hilo halitapatikana isipokuwa tu kwa kuwa na imani angavu inayooteshwa katika nyoyo, imani itakayowakomboa wanadamu watokane na utumwa wa kuabudu madhalimu na masanamu sawa yawe ni mawe au binadamu.

Uhuru katika Uislamu, enyi ndugu zangu, unakuwa katika sura ya utumwa. Uhuru una maana ya kuifanya nafsi yako kuwa mtumwa wa Mwenyezi Mungu pekee katika mwelekeo wa moyo wako na itikadi zake, katika mienendo ya fikra zako na utashi wake, katika kauli zako na vitendo vyako na katika kanuni zinazoitawala jamii.

شبكة الألوكة - قسم الكتب

Uhuru mwingi wanaoukodolea macho watu katika wakati wa sasa ni utumwa tu katika mtazamo wa Uislamu. Chukueni mazingatio kwa kile kinachoitwa demokrasia hivi leo. Watu wanaona kuwa kuipata demokrasia ndio kilele cha uhuru ambao watu wanaweza kuupata hivi leo. Mataifa huhangaika kumchagua rais wan chi, kama ambavyo wanachagua wawakilishi wanaoutungia umma sheria watakazo na kufuatilia kwa karibu vyombo vya utendaji katika nchi zao. Haya katika mtazamo wa Uislamu ni utumwa wa wanadamu kuwaabudu wanadamu wenzao na wanadamu kuwafanya miungu wanadamu wenzao.

Si katika haki ya wanadamu kututungia sheria ambazo Mwenyezi Mungu hakuziidhinisha, na si katika haki yao kuyaendesha maisha kwa fikra zao tu. Iwapo watafanya hivyo, basi wao ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu amewashutumu Wayahudi na Wakristo kwakuwa waliwafanya wanazuoni na watawa wao kuwa miungu badala ya Mwenyezi Mungu. Na tumefahamu kupitia tafsiri ya Mtume, Mwenyezi

شبكة الألوكة - قسم الكتب

Mungu amfikishie rehema na amani, kuwa maana ya kuwafanya miungu badala ya Mwenyezi Mungu ni Wayahudi na Wakristo kuwafuata wanazuoni na watawa wao katika kuhalalisha mambo aliyoyaharamisha Mwenyezi Mungu na kuharamisha mambo aliyoyahalalisha Mwenyezi Mungu pamoja na kuwa wao wanafuata sheria zao kwa njia moja au nyingine. Iwapo ni hivyo, ni vipi basi mataifa ya sasa yanapowapa wawakilishi wa wananchi (wabunge) uhuru wa moja kwa moja katika kutunga sheria watakazo? Wamehalalisha riba, zinaa, ulawiti, utoaji mimba na pombe. Kila kitu katika mtazamo wa mataifa ya kidemokrasia kinaweza kuangaliwa upya na kubadilishwa. Huu katika mtazamo wa Uislamu ni utumwa tena utumwa mkubwa unaowafanya wanadamu kuwa watumwa wa wanadamu wenzao. La ajabu ni kwamba mataifa mengi yanaona kuwa hayo ni kilele cha uhuru.

Uhuru wa kweli una maana ya kumnyenyekea Mwenyezi Mungu pekee, kuchukua mfumo wake na si mfumo wa mwengine na kujihukumu kwenye

شبكة الألوكة - قسم الكتب

sheria zake badala ya sheria na kanuni nyingine. Watu wakiukataa utumwa huu wa kumwabudu Mwenyezi Mungu Mmoja na wa Pekee, basi wao bila ya shaka yoyote watajifanya wawe watumwa wa viumbe vilivyo sawa na wao ambavyo ni wanadamu wenzao au viumbe ambao ni duni kuliko wao. Ni jambo baya kwa mwanadamu kujifanya mtumwa wa kumwabudu kiumbe kama yeye asiyedhuru wala kunufaisha bali pengine haoni wala hasikii.

Anayestahiki kuabudiwa ni yule aliesifika na sifa za kweli za uungu. "**Sema: Sifa njema anazistahiki Mwenyezi Mungu na amani iwashukie waja wake alio(wa)teua. Hivi Mwenyezi Mungu ni bora zaidi au (bora zaidi ni) wanavyovishirikisha? Au (bora zaidi) ni yule aliyeumba mbingu na ardhi na akakuteremshieni kutoka mawinguni maji (mvua) tukaotesha kwayo bustani zenye kufurahisha, hamkuweza kuotesha miti yake. Hivi kuna Mungu mwengine pamoja na Mwenyezi Mungu? Bali wao ni watu wanaolinganisha. Au (bora zaidi)ni yule aliyeifanya ardhi kuwa tulivu na**

شبكة الألوكة - قسم الكتب

**kuweka katikati yake mito na akaiwekea ardhi milima na akaweka kati ya bahari mbili kizuizi. Hivi kuna mungu mwengine pamoja na Mwenyezi Mungu? Bali wengi wao hawajui. Au (bora zaidi) ni yule anayemjibu mwenye shida wakati amuombapo na anakuondoleeni mabaya na kukufanyeni nyinyi makhalifa wa duniani. Hivi kuna Mungu mwengine pamoja na Mwenyezi Mungu? Ni uchache sana mnavyo onyeka. Au (bora zaidi) ni yule anayekuongozeni katika giza la bara na baharini na yule apelekaye pepo zikibashiri (habari njema ya mvua) mbele ya rehema zake? Hivi kuna Mungu mwengine pamoja na Mwenyezi Mungu? Ametakasika Mwenyezi Mungu na (yale makafiri) wanayoyashirikisha (naye). Au (alliye bora zaidi) ni yule aliyeanza kuumba halafu atarudia, na ambaye anakupeni riziki kutoka mbinguni na ardhini? Hivi kuna Mungu mwengine pamoja na Mwenyezi Mungu? Sema: Leteni hoja yenu ikiwa nyinyi ni wakweli**". Sura An-naml (27), aya 59-64.

شبكة الألوكة - قسم الكتب

Sifa njema anazistahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe.

www.alukah.net
شبكة الألوكة
شبكة الألوكة - قسم الكتب

هذا الكتاب منشور في

شبكة الألوكة

www.alukah.net